**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU SUMBAWANGA**

P.O Box 350 Sumbawanga, simu 0759298359, 0714189701, Email: sumbawangatc@moe.go.tz

Unapojibu taja SBA/CCU/JI/153/25 Tarehe: 04.06.2026

Ndugu ………………………………………

…………………………………………………

…………………………………………………

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI MWAKA WA MASOMO 2026/2027

### UTANGULIZI

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa kozi ya Sayansi na Hisabati Mafunzo haya yatachukua muda wa miaka miwili, kwa wale watakaokaa chuoni moja kwa moja na Miaka **(03 hadi 04)** kwa wale watakaosoma Stashahada ya Ualimu kwa njia ya Masafa.

**CHUO CHA UALIMU SUMBAWANGA** kipo mkoani Rukwa katika Manispaa ya Sumbawanga.

Pamoja na barua hii nakutumia maelekezo ya kujiunga na Chuo (Joining Instruction) ikiwa pamoja na fomu ya uthibitisho wa afya yako kuwa inakuruhusu kuhudhuria mafunzo ya Ualimu (Ijazwe kabla ya kufika chuoni). Baada ya kusoma maagizo na kuyaelewa vizuri, kama unakubali kujiunga na mafunzo hayo katika Chuo hiki jiandae haraka kwa kuzingatia maelekezo yote yaliyotolewa ili uripoti chuoni tarehe iliyopangwa.

**A: TAREHE YA KURIPOTI CHUONI**

Tarehe ya kuripoti ni **17 Agosti, 2026**, unapaswa kufika Chuoni siku iliyopangwa. Ukifika chuoni muone Msajili wa Wanachuo ambaye atakupokea na kukupa maelekezo zaidi. Wanachuo wa Masafa watapaswa kusajiliwa rasmi na kuanza masomo yao haraka iwezekenavyo. Mwisho wa kuripoti chuoni ni tarehe **31/08/2026.**

**B: MAHITAJI MUHIMU**


Karo/Ada ni **Tsh 450,000**/= kwa mwaka, Karo inaweza kulipwa mara moja au mara mbili yaani **Tsh 225,000/=** kwa kila muhula.


Utalipa kupitia **Mfumo wa kielektroni wa malipo ya Serikali (GEPG),**ambapo utatakiwa kuchukua namba hiyo kwa mhasibu wa Chuo ili uweze kulipa ada ya Chuo. Unaweza kufanya mawasiliano na mhasibu kwa namba **0753011287** ili kupatiwa namba ya malipo (Control Number) ukiwa nyumbani. Baada ya kupewa namba ya malipo utafanya malipo katika Benki yoyote iliyo karibu nawe au kwa kutumia mitandao ya simu kama M-PESA, TIGO PESA, AIRTEL MONEY n.k

Kumbuka, utatakiwa kuja na hati ya malipo ambayo utaikabidhi kwa mhasibu ili upatiwe Stakabadhi ya malipo.

**C: SARE YA CHUO:**
Utatakiwa kuwa na sare za Chuo (Buluu nyeusi (darkblue) na suti nyeusi) kama ifuatavyo:

**(a) WASICHANA**
Sketi ndefu juu kidogo ya kisigino rangi Buluu na nyeusi yenye rinda box nyuma (Kitambaa kizito) na shati ya mikono mirefu rangi ya light blue (Aina ya Kangaroo bluu bahari). Koti jeusi lisilo na mpasua nyuma**,** tai nyeusi**. Kwa Waislamu wataruhusiwa kuvaa hijabu ya light blue ambayo haina urembo wowote.** Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba, visivyo na kisigino kirefu, soksi nyeupe, pamoja na T-Shirt mbili zenye nembo ya Chuo **Tsh 30,000/=** zinapatikana Chuoni.





Mbele Nyuma

**(b) WAVULANA**

Suruali (Kitambaa kizito) rangi buluu na nyeusi, shati la mikono mirefu rangi ya light blue (aina ya kangaroo blue bahari).

i. Viatu vya ngozi, rangi nyeusi, vya kufunga na kamba, visivyo na kisigino kirefu.

ii. Koti rangi nyeusi aina ya suti (kujikinga na baridi)

iii. Soksi rangi nyeupe na tai nyeusi.

iv.T-Shirt mbili zenye nembo ya Chuo **Tsh 30,000/=** zinapatikana Chuoni.

**NB:** *Ili kuleta usawa wa rangi ya suti, na mishono inayofanana, unashauriwa uje ushonee sare kwa fundi aliyepo hapa Chuoni kwa gharama ya TSh 100,000 tu. Gharama hizi zitahusu Suruali/sketi 2, mashati 2, koti 1 na tai 1.*

***SARE ZOTE ZITASHONWA AU KUPATIKANA HAPA HAPA CHUONI ILI KULETA USAWA WA RANGI NA MISHONO***

**D: MAHITAJI MUHIMU**

Kumbuka wanachuo wote watakaa bweni na Chakula kitatolewa chuoni bila gharama yoyote. Hivyo unatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo;

i. Vyombo vya chakula na matumizi mengine mfano; Sahani, Bakuli, Kikombe (Vyote vya udongo), na kijiko.
ii. Blanketi la kujifunika (Kuna baridi)
iii. Shuka 3, moja jeupe na la pili Pinki na la tatu rangi yoyote kwa ajili ya kulalia.
iv. Chandarua
v. Nguo za michezo; tracksuit (rangi ya light blue) na raba. Ifahamike kuwa, wakati wa michezo kila mwanachuo anatakiwa kuvaa sare za michezo.
vi. Squezer,brush za kusugulia choo na fyekeo kwa wavulana
vii. Reki, mopa na fagio ngumu kwa wasichana

**E. MAHITAJI MENGINE YA LAZIMA**

**(i) Wanachuo Wanaosoma Stashahada ya Ualimu Kozi ya Sayansi na Hisabati kwa miaka Miwili:**

Unatakiwa kuja na michango ifuatayo:

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| 1 | Huduma ya Kwanza | 10,000/= | Kwa mwaka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2 | Ukarabati na matengenezo | 25,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Usajili na Kitambulisho | 20,000/= | Italipwa Mara moja mwaka1 |
| 4 | Serikali ya wanachuo | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 5 | Kukodi godoro | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 6 | Elimu ya michezo | 25,000/= | Kwa mwaka |
| 7 | Ulinzi | 25,000/= | Kwa mwaka |
| 8 | Matumizi ya ICT/TEHAMA | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 9 | Usafi, Mazingira na EK | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 10 | Bima ya afya | 50,400/= | Kwa mwaka kwa wasio na Bima ya Afya |
| | **JUMLA TSH** | **200,400** | |

**(ii) Michango Mingine kwa Wanachuo Wanaosoma Stashahada ya Ualimu Kozi ya Sayansi na Hisabati kwa njia ya Masafa Miaka (03 hadi 04)**

| **Na** | **Aina ya mchango** | **Kiasi** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| **1** | Serikali ya wanachuo | 5,000/= | Kwa mwaka |
| **2** | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Kwa mwaka |
| **3** | Usafi wa mazingira | 20,000/= | Kwa mwaka |
| **4** | Ufuatiliaji na uendeshaji wa Mafunzo | 40,000/= | Kwa mwaka |
| **5** | Usajili na kitambulisho | 20,000/= | Kwa mwaka wa kwanza tu |
| **6** | Michezo | 30,000/= | Kwa mwaka |
| **7** | Ukarabati | 25,000/= | Kwa mwaka |
| | **JUMLA** | **150,000/=** | |

Fedha zote zilizotajwa katika kipengele (E) za mahitaji mengine ya lazima, zilipwe kwenye akaunti ya Chuo ambayo ni **Chuo Cha Ualimu Sumbawang**a Benki ya **CRDB** akaunti namba **01J1068657500,** na si vinginevyo

***"Tafadhali, Fedha ya Ada isiingizwe katika akaunti ya Michango"***

**F: VIFAA VYA MASOMO**

Unapaswa kuja na vifaa vifuatavyo;

i. Daftari 14 (Counter books 2quire)
ii. Kalamu za wino (Red, blue/black na kalamu ya HB)
iii. Rimu mbili (2) za karatasi A4 kwa mwaka
iv. Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)
v. Fedha kwa ajili ya mahitaji madogomadogo (Kwa matumizi binafsi, usafi na kwa ajili ya kununulia vifaa vya kutengenezea zana za kufundishia na kujifunzia)

**G: SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO**

Mwanachuo mara afikapo Chuoni atapaswa kufuata na kuzingatia taratibu na sheria za Chuo, mwanachuo atajaza fomu maalumu kukubaliana na sheria hizo.

**H: VYETI NA VITAMBULISHO**

Utasajiliwa kama utakuwa na vitu **vyote vilivyotajwa** pamoja na vifaa vifuatavyo:

i. Vyeti cha kumaliza kidato cha **NNE na SITA** (Original) chenye picha yako na muhuri wa shule yako yaani **leaving certificate**.
ii. Vyeti vya **BARAZA LA MITIHANI** vya kidato cha **NNE na SITA,** Na kwa walimu wanaojiendeleza (Bweni na kwa njia ya Masafa) waje na cheti cha kidato cha nne na cheti cha astashahada ya ualimu daraja la IIIA (**Grade IIIA**) njoo na (**Original Academic Certificate)** Usije na photocopy**.** Ukija na photocopy hutasajiliwa
iii. Barua ya kuitwa Chuoni (Joining instructions)
iv. Fomu iliyojazwa kuthibitisha afya yako kuruhusu kuendelea na mafunzo (Ijazwe katika hospitali ya Serikali).
v. Cheti halisi cha kuzaliwa.

**I: HALI YA CHAKULA**

Chuo hutoa chakula kizuri kwa wanachuo wote. Chuo hakina uwezo wa kugharamia au kutoa chakula maalum (Special diet) kwa wanachuo wenye matatizo.

**J: USAFIRI**

Baada ya kupata barua hii fanya mipango ya usafiri kuja chuoni. Chuo kipo ndani ya **Sumbawanga Manispaa (**Eneo la PITO), **km 7** toka kituo kipya cha mabasi kilichopo Katumba katika Kijiji cha Pito.

Kama unatokea njia ya **Mbeya** au **Mpanda** unatakiwa kushuka kituo cha mabasi/stendi ya katumba na kuchukua usafiri kuja chuo kilipo.

Karibu sana Chuo cha ualimu Sumbawanga.

**Mkuu wa Chuo**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU SUMBAWANGA
S. L. P. 350
SUMBAWANGA

# GOVERNMENT OF TANZANIA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To Medical Officer

……………………………….
………………………………

From ……………………..

………………………………

**PART A**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1 a) Eye-sight
 b) Hearing
 c) Speech
 d) Venereal diseases
 e) Leprosy
 f) Limbs
 g) Epilepsy

 2. Neuroses
 3. Other serious diseases

B: Blood Group

Signature …………………

Date ……………………… Official stamp ………………….

……………………………………………………………………………

**PART B MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by Government medical officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for pursuing full time teacher education course.

I. a) Eye- Sight ………………………………………………………………….
 b) Hearing ………………………………………………………………….
 c) Limbs …………………………………………………………………..
 d) Speech …………………………………………………………………..
 e) Leprosy …………………………………………………………………..

II. Neuroses ………………………………………………………………….

III. Other serious diseases …………………………………………………

IV. Pregnancy …………………………………………………………………..

Signature ………………………….

Date ………………………. Official stamp…………………………..